**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWALIMU J K NYERERE

**Juni, 2023**

**Songwe**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu : 0655404106**

**Mkuu wa Shule : 0753404106**

**Makamu Mkuu wa Shule : 0758971636**

**Matron/Patron : 0753069995**

**Shule ya Sekondari MWALIMU J K NYERERE**

**S.L.P 188,**

**Tarehe 13/06/2023.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWALIMU J K NYERERE HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA MKOA WA SONGWE MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGK, HKL, CBG

Shule ya sekondari MWL.J.K.NYERERE ipo Mkoa wa Songwe katika Halmahauri ya Mji Tunduma umbali wa kilomita kumi na tano(15) kutoka kituo kikuu cha mabasi Mpemba. Shule ipo kandokando mwa barabara kuu ya Tunduma-Sumbawanga.

Sambamba na barua hii unatakiwa kuyasoma na kuyaelewa maelezo yaliyo ambatanishwa kwa umakini. Pia unapaswa kuyatimiza maagizo yote mara mwanao ajapo shuleni.

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja kujiunga na shule hii. Aidha nakukumbusha kujihadhari na matapeli pia mambo mbali mbali yanayoweza kuathiri afya yako kwa kuzingatia miongozo ya afya kama inavyotolewa na Wataalamu wa afya uwapo safarini.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

Wako katika Elimu na Malezi.



…………………………………………..

**Mwl. CHRISTOPHER HARRY NKEMBO**

**MKUU WA SHULE**

**(0753404106 )**

.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

Ili kuepuka usumbufu epuka mishono ya kihuni kama vile suruali za kubana na fupi. Zingatia rangi ulizoelekezwa.

- Suruari 2 (Dark blue 1) na (Damu ya mzee, “maroon” 1) *Angalia picha ukurasa wa mwisho.
- Mashati mawili meupe mikono mirefu
- Tai mbili za mistari mieupe kulingana na rangi ya suruali (pundamilia) .
- Soksi jozi mbili (Nyeusi)
- Sweta la blue1
- Viatu vyeusi vyenye kisigino jozi mbili
- T-shirt ya kola moja (Blue).

**2. SARE ZA NJE YA DARASANI**

- Suruali mbili rangi ya khaki.
- Traki suti mbili nyeusi na dark blue
- Bukta za mazoezi mbili rangi ya blue
- Raba za michezo ama viatu *njumu* jozi mbili
- T-shirt shingo ya duara nyeupe mbili

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Folder file moja
ii. Picha mbili passport size akiwa amevaa shati nyeupe (background blue)
iii. Disect kit kwa wanafunzi wanaosoma somo la Biolojia

iv. Laboratory coat moja kwa wanafunzi wa sayansi
v. Nakala za vyeti vya kitaaluma (Result slip na living certificate)
vi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

**VIFAA VYA DARASANI**

i. Madaftari tisa 3Q na 4Q
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe ni futi $2\frac{1}{2}$ x 6
vi. Mashuka Jozi 2 ya rangi blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 1 (20L) na ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 3 ya ndani (soft bloom, hard bloom na brush za chooni).

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**FEDHA HII INGIZWE KWENYE AKAUNTI NA 61502300086 MWALIMU J K NYERERE SECONDARY (NMB BANK)**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule CHRISTOPHER HARRY NKEMBO**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** 

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0753404106**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0758971636**
- **Mwandamizi Taaluma : 0767714612**
- **Mwandamizi Malezi : 0768456494**

## UTHIBITISHO WA URAIA WA MTANZANIA

Nadhibitisha kuwa…………………………………………………………... (jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa

Baba yake (jina kamili) ……………………………………………………………………………

Amezaliwa katika mkoa wa ……………………………….…. Wilaya ya ……………………

Tarafa ya ………………………………………………. Kata ya ………………………………

Mama yake (jina kamili) ………………………………………………………………………

Amezaliwa katika kata ya ……………………………………….. Wilaya ya …………………

**…………………………………………………………………**

**MKUU WA WILAYA**

**NB**: kila mwanafunzi atalazimika kuishughlikia hati kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni.

**AU LETA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA BADALA YA FOMU HII**.

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MWALIMU J K NYERERE SECONDARY SCHOOL

P.O. Box 188,

**TUNDUMA**.

Date: ………………………………

To:

THE MEDICAL OFFICER,

…………………………………………….

…………………………………………….

…………………………………………….

Please examine ……………………………………………………………………………..

As to her fitness for pursuing further education at this school.

- Hemoglobin ……………………………………………………………………………
- P.V. Blooding……………………………………………………………………………
- (A) Blooding ……………………………………………………………………………

(B) Hearing …………………………………………………………………………………

- Blood Pressure…………………………………………………………………………
- Urine for Sugar tests……………………………………………………..……………
- Stool for routine examination…………………………………………………………
- Asthma ……………………………………………………………………………………
- Skin diseases ……………………………………………………………………………
- Leprosy ……………………………………………………………………………………
- Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………………
- Employs ……………………………………………………………………………
- Deformity ……………………………………………………………………………
- Mental problem …………………………………………………………………………
- Comments ………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

…………………………………………….

**DESIGNATION**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**
**SHULE YA SEKONDARI MWALIMU J K NYERERE**

FOMU YA KUKUBALI NAFASI

## a. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ijazwe na mwafunzi mwenyewe)

Jina kamili[kama alivyo sajiliwa darasa la saba]…………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa…………….…Kabila…………………dini na dhehebu…………………

shule nitokayo…………….…………Mahali niishipo…………………………..

Mkoa………………………..…Anuani…………………………………………

Jina la baba/mlezi…………………………………….kazi yake…………………………..

Jina la mama/mlezi…………………………………...kazi yake……………………………

Wazazi/walezi wanaishi (wapi)…………………………pamoja/au wametengana……………

Anuani ya mzazi/mlezi……………………………..simu……………………………………

Wakati wa likizo nitakuwa kwa (mtaje)……………………………wapi………………………

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi;

Sahihi ya mwanafunzi……………………………….tarehe……………………………….

KUKUBALI (mwanafunzi mwenyewe ajaze)

Mimi…………………………………………………………………………nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivyo ninakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe iliyopangwa.

**b. IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI**

Mimi……………………………………………………………. ambaye ni ……………………. wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule katika fomu ya kujiunga. Nipo tayari ajiunge na shule hii, naahidi kumpa mahitaji yote ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitikia wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika.

Anuani yangu ya kudumu……………………………..simu………………………………

Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Nathibitisha Taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli

Sahihi ya mzazi /mlezi……………...